

Nduni za Fasihi ya Watoto: Mifano Kutoka katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto nchini Tanzania

Edith B. Lyimo

Ikisiri

Fasihi, andishi au simulizi, ili iweze kufikisha ujumbe uliokusudiwa, lazima izingatie kanuni za utunzi zinazoendana na hadhira lengwa. Fasihi ya watu wazima ni tofauti na fasihi ya watoto ijapokuwa zote huweza kuwa na dhima zilizile za kufundisha, kuburudisha, kuonya, kuadibu, kufundisha lugha na kadhalika. Fani ni kati ya vipengele vinavyotofautisha fasihi ya watu wazima na fasihi ya watoto. Makala haya yanabainisha na kujadili nduni bainifu za fasihi andishi ya watoto. Lengo kuu la makala haya ni kuonesha nduni mbalimbali zinazotawala fasihi andishi ya watoto na hivyo kuitofautisha na fasihi andishi ya watu wazima.

1.0 Utangulizi

Katika makala haya dhana ya mtoto na fasihi ya mtoto ni dhana muhimu ambazo bila kufafanuliwa, makala hayataeleweka kwa urahisi. Hivyo, sehemu hii itafafanua pamoja na kutoa usuli kuhusiana na dhana hizi. Mtoto ni dhana ambayo imekuwa ikipata fasili mbalimbali kulingana na muktadha wa matumizi yake. Lyimo (2014) anasema kuwa neno mtoto linaweza kufasiliwa kwa kutumia vigezo mbalimbali vya kijamii, kiimani, kiumri, kibiojia na kadhalika. Hii ina maana kuwa ufafanuzi wa dhana hii huweza kupatikana kwenye muktadha wa mahusiano ya uzazi, utu uzima, kitu kizima, kiumbe kinachozaa, kitu kinachochipusha, kutotoa au kutoa kiumbe. Katika mazingira ya wazungumzaji, wakati mwingine, kuwapo kwa kitu kikubwa na kidogo wazungumzaji hujikuta wakitumia dhana ya -toto. Mfano mgomba umetoa mtoto (mgomba umechipua), kuku ana watoto/ametotoa (kuku aliyekuwa anaatamia ana vifaranga), mtoto wa ng'ombe (ndama) na kadhalika. Katika muktadha wa kuamini katika Mungu, mwanadamu anaitwa mtoto wa Mungu (yaani ametokana na Mungu, ni mdogo kuliko Mungu, baba yake ni Mungu). Kwa mantiki hii, mtoto ni kama kiumbe au kitu kinachotokana na kitu kingine kikubwa. Kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Oktoba 1996, dhana ya mtoto inaelezwa kuwa ni mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na minane. Aidha, ni mtu anayehitaji kupata uangalizi wa mtu aliyepévuka kiakili, kimwili na kiroho kwa maana kwamba hajafikia kiwango cha kuweza kufanya maamuzi ambayo ni sahihi au yanayokubalika kulingana na taratibu za jamii.

Fasihi ya watoto kama wanavyoeleza wataalamu mbalimbali (Nodelman, 2008; Lyimo, 2014) ni dhana inayotumika kumaanisha kazi za kifasihi ambazo zimetungwa kwa ajili ya kusomwa au kutendwa na watoto. Kazi hizi ni pamoja na kazi za fasihi simulizi kama vile nyimbo, semi, na simulizi; na kazi za fasihi andishi kama vile riwaya, tamthiliya na ushairi. Kwa kiasi kikubwa fasihi ya

watoto imesheheni vipengele vya sanaa jadiya kama vile mambo ya majini, mazimwi, sihiri au uchawi, nyimbo, michezo, matambiko, visakale, visasili, hekaya, methali, na vitendawili (Ruterana, 2012). Kutokana na fasihi ya watoto kutawaliwa na sifa hizi za fasihi simulizi, vipera vyake au tanzu zake huingiliana (Mulokozi, 1989) kwa madhumuni mbalimbali. Baadhi ya madhumuni ya kuingiliana ni kwa ajili ya kuwaburudisha watoto na pia kufikisha vizuri ujumbe aliokusudia mtunzi kwa hadhira yake. Tofauti na ilivyo fasihi ya watu wazima ambayo hutungwa na watu wazima na walengwa wake ni watu wazima, fasihi ya watoto nchini Tanzania na duniani kote waandishi wake wengi ni watu wazima lakini walengwa wake ni watoto. Hali hii wakati mwingine huweza kuwafanya watunzi kujisahau na kujikuta wakikiuka kaida za utunzi na hivyo kuingiza pia mitazamo, mawazo au itikadi na dhamira zinazohusu waandishi hawa au kundi la watu wazima. Hamasa ya watu wazima kutunga kazi za fasihi za watoto huweza kutokana na ukweli kwamba fasihi licha ya kuwaburudisha watoto, ni nyenzo ambayo inatumika katika kuwajenga watoto kimaadili, kiakili na uwezo wao wa lugha (Ruterana, 2012). Watoto hutegemea sana kuelekezwa na watu wanaowazunguka au na nyenzo zinazopatikana katika mazingira yao wanayoishi au kusomea zikiwapo kazi za fasihi (Lyimo, 2014).

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) dhima ya fasihi, iwe simulizi au andishi katika jamii hufanana isipokuwa hutofautiana katika vipengele vya utunzi, uwasilishwaji, mazingira ya uwasilishaji, hadhira, umri, umilikaji, tanzu, lugha, kubadilika, wahusika, markebisho na uhifadhi. Kwa kuchunguza vipengele hivi, ni dhahiri kuwa kutofautiana kwa kazi za kifasihi hutegemea zaidi kipengele cha fani.

Wamitila (2003) anaeleza fani kama dhana inayotumika kuelezea muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake. Wamitila anaendelea kueleza kuwa fani huelezea mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui. Akifafanua mawazo haya Senkoro (2011) anaeleza fani katika fasihi kuwa ni ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kazi yake kupitia vipengele vya wahusika, lugha, muundo na mtindo. Katika uchanganuzi wa fani wanafasihi akiwamo Wamitila (2008) wanajumuisha pia kipengele cha mandhari.

1.1 Wahusika katika Fasihi

Wahusika wa kifasihi ni watendaji au watendwaji wa kazi ya fasihi. Hawa wanaweza kuwa binadamu, wanyama wengine wasio na urazini, ndege, wadudu, mimea, mawe, upepo na kadhalika. Kwa kifupi wahusika wanaweza kuwa viumbe wenye uhai au wasio na uhai ambao katika kazi ya fasihi hupewa uhai. Wahusika hawa hupewa uhusika kulingana na kile alichokikusudia mtunzi. Mtunzi huamua kutumia wahusika wa aina fulani kulingana na kile anachotaka kiwasilishwe, hadhira yake pamoja na muktadha wa uwasilishaji.

1.2 Lugha katika Fasihi

Lugha kama inavyofafanuliwa katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2013) ni “Mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana ambao hutumiwa na watu wa taifa au kundi fulani kwa ajili ya kuwasiliana.” Kamusi hii pia inafafanua aina mbalimbali za lugha kimuktadha na kimatumizi. Mathalani, tunapata lugha ya taifa, lugha rasmi, lugha ya ishara (lugha ya mawasiliano ambayo haitumii sauti au maneno). Katika muktadha huu, picha, michoro, rangi na ishara za kimawasiliano pia ni lugha. Lugha ya kifasihi hutofautiana na lugha ya kawaida kwa sababu lazima mtunzi ateue maneno, tungo na tamathali za semi ambazo zitaleta athari katika kazi yake.

1.3 Mandhari katika Fasihi

Wamitila (2008) anafasili mandhari kama wakati na mazingira ambayo ndio msingi katika uandishi wa kazi za kifasihi. Katika uanishashaji wa mandhari Wamitila anasema kuwa kuna mandhari za kijiografia (mandhari za kihalisia), kihistoria (mandhari zinazokiuka na masuala ya kihistoria), kidhanifu au kinjozi (mandhari inayokiuka uhalisia), kiishara (mandhari zinazotokana na ishara), kidokezi (mandhari zinazoishia na kudokeza) na kiajinabi (mandhari zinazokiuka sifa za kawaida). Ijapokuwa Wamitila ameanisha mandhari hizi, tunaweza kupata aina mbili kuu ambazo ni mandhari halisi na mandhari za kinjozi au dhahania ambazo huwa na dhima mbalimbali.

1.4 Muundo katika Fasihi

Muundo na mtindo ni vipengele vya fani ambavyo vinawachanganya sana watu wengi hasa ambao si wanafasihi (Senkoro, 2011). Akijaribu kuvitofautisha vipengele hivi, Senkoro (keshatajwa) anasema kuwa muundo wa kazi ya fasihi ni mpango na mtiririko wa kazi hiyo kwa kuzingatia visa na matukio. Senkoro anabainisha miundo miwili mikuu ambayo ni muundo wa moja kwa moja na muundo wa kiuchangamani. Akifafanua miundo hii Senkoro anatoa mfano wa muundo wa moja kwa moja ambao mfano wake ni kumwona mhusika akizaliwa, akikua, akichumbia au kuchumbiwa, kuwa katika ndoa kuzeeka na kufa. Mfano wa muundo wa kiuchangamani anaoutoa Senkoro ni wa kiurejeshi ambao huweza ama kumrudisha nyuma msomaji msikilizaji au mtazamaji kutika mpangilio wa matukio yake au kipeleka mbele hadhira ya kazi hiyo (Senkoro, 2011:24).

1.5 Mtindo katika Fasihi

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia* (2003), mtindo ni dhana inayoeleza jinsi mwandishi anavyojieleza mwenyewe. Kwa mujibu wa wanazuoni na wanataaluma walioshughulikia au kuchambua mitindo katika kazi mbalimbali za kifasihi kama vile Enkvist, mtindo una dhana mbalimbali. Baadhi yake ni kama

vile mtindo ni utofauti, ukiushi, uteuzi, nyongeza, mazoea au kaida na kadhalika (Enkvist, 1973; Halliday na Hasan 1976; Kahigi, 1997; Lyimo, 2004). Kwa ujumla, mtindo ndio unaotuwezesha kwa kiasi kikubwa kupata tofauti kati ya kazi moja ya fasihi na nyingine au tanzu moja na nyingine kwa sababu huhusika zaidi na NAMNA au JINSI; jinsi mtunzi alivyowaumba wahusika wake, jinsi alivyoanza kisa chake, jinsi alivyomalizia kisa chake, jinsi alivyotumia lugha, jinsi alivyowasilisha ujumbe wake kwa hadhira aliyoikusudia na kadhalika.

2.0 Nduni Bainifu za Fasihi ya Watoto

Wataalamu mbalimbali hasa walioshughulikia fasihi ya watoto (Kahigi, 1995; Narahara, 1998; Blaska, 2004; Nodelman, 2008; Wamitila, 2008) wanasema kuwa kuna sifa ambazo hupambanua fasihi ya watoto na fasihi ya watu wazima na hivyo kuwa ni utanzu. Hii ina maana kwamba kuna sifa mtambuka zinazozitofautisha kazi za fasihi ya watoto na kazi za fasihi ya watu wazima kiasi cha kuzifanya kuwa sifa za jumla kwa kazi zote na mahususi kwa fasihi ya watoto. Katika utafiti huu, tumejaribu kuchunguza tofauti zilizopo kati ya kazi za fasihi za watoto ya Kiswahili na za Kiswahili za watu wazima kwa kulinganisha baadhi ya vipengele vya fani na maudhui. Vipengele hivyo ni hadhira, lugha, wahusika, muundo na mtindo.

2.1 Hadhira Kuu ya Kazi za Fasihi ya Watoto ni Watoto

Wakati fasihi ya watu wazima hadhira yake ni watu wazima, kwa upande wa fasihi ya watoto hadhira yake au walengwa wakuu ni watoto. Katika kitabu cha *Tabu wa Taire, Kalikalange Mtoto wa Ajabu, Mji wa Mawe, Sababu Mimi ni Mwanamke, Laba Msichana Shujaa* ijapokuwa mtu yeyote anaweza kupenda kusoma vitabu hivi, hadhira lengwa ni watoto. Kwa kuchunguza vitabu hivi tunaona kuwa kuna mambo ambayo watoto huyafurahia zaidi kuliko watu wazima. Mathalani picha, lugha rahisi, michezo ya watoto na masuala ya kifantasia. Hii inatokana na ukweli kwamba waandishi wanataka watoto waburudike na pia wapate mafunzo fulani yaliyokusuduwa ndani ya vitabu hivyo. Kwa mfano, katika *Tabu wa Taire* mwandishi anataka watoto wawatii wakubwa wao kwa kufuata maelekezo wanayopewa. Pamoja na kuwa yapo mambo mengine ambayo huwalenga pia wazazi na walezi, jinsi ya uwasilishaji hujikita sana katika kumwangukia mtoto. Kutokana na sifa hii, maudhui pamoja na fani inayotumika lazima iendane na watoto (Wamitila, 2008) na iwe na mtazamo wa watoto (Nodelman, 2008). Hii ina maana kwamba mtunzi anapotunga kazi yake lazima azingatie saikolojia ya watoto. Hana budi kuandika kuhusu mada ambazo zinawasisimua watoto huku akijua ni mambo gani ambayo watoto wanayafurahia au wanayachukia, na ni mambo gani yatawajenga watoto kiakili na kijamii, na kuepuka mambo ambayo yatawaletea watoto athari hasi. Kazi nyingi za watoto, tofauti na za watu wazima zina uhuru mkubwa wa wahusika bapa na visa vya wanyama, ndege, wadudu, mimea na binadamu. Pamoja na uhuru huo, matendo

ya wahusika hao lazima yazingatie hadhira ya watoto. Visa kama vya sungura na fisi, mbwa na paka, kuku na mwewe, paka na panya, simba na binadamu na vinginevyo; pamoja na matumizi mbalimbali ya vitu na kadhalika, ndivyo ambavyo huwafurahisha zaidi watoto kuliko watu wazima. Watoto hudhani na kuamini kuwa visa hivyo ni vya kweli kutokana na umri wao mdogo wa kutofautisha mambo ya kweli au ulimwengu halisi na mambo ya kufikirika au ulimwengu wa kubuni.

2.2 Watoto ndio Nguli na Wahusika Wakuu

Wahusika wakuu katika kazi za watoto zilizochunguzwa ni watoto wenyewe. Katika vitabu 12 vya watoto vilivyochambuliwa, ambavyo wahusika wakuu ni watoto na ni nguli ni pamoja na: *Mpishi Mwenye Kibiongo*, *Kipofu Mwenye Miwani Myeusi*, *Sababu mimi ni Mwanamke*, *Laba Msichana Shujaa Mji wa Mawe*, *Kalikalange Mtoto wa Ajabu na Safari ya Mzimuni*. Katika vitabu vya *Bahati na Mumewe*, *Kirisongo*, *Chifu Mahawanga* na *Wawindaji Watatu*, wahusika wake wakuu ni watoto ambao wanataka kuvuka daraja na kuingia katika utu uzima wa kimajukumu. Baadhi ya wahusika katika vitabu hivi wanataka au wanapendekezwa kuoa au kuolewa.

Pamoja na kwamba wahusika wakuu/nguli wa fasihi ya watoto ni watoto wenyewe, wapo waandishi ambao hawazingatii kipengele hiki. Matokeo yake watoto hujikuta wakioneshwa zaidi matendo yanayofanywa na watu wazima na hivyo kuiga matendo hayo katika vitabu vinavyoaminiwa kuwa vitabu vya watoto. *Wawindaji Watatu* ni moja kati ya kazi za aina hii. Ijapokuwa mtunzi alikusudia kumfundisha mtoto kuhusu ubaya wa tamaa, anajikuta akimsahau mtoto na kuishia kuelezea tu masaibu ya wawindaji watatu hadi mwisho, bila kumpa tena mtoto nafasi ya kutoa angalau mtazamo wake. Hali hii husababishwa na mazoea au kushindwa kuzima itikadi aliyonayo mwandishi au soko huria ambalo humfanya mwandishi wakati mwingine afanye kile ambacho anaona kinamfaa yeye bila kufungwa sana na kanuni (Lyimo, 2014). Kwa ujumla, wahusika wakuu au wahusika wengi watendaji au watendwaji katika fasihi ya watoto ni watoto, ijapokuwa pia haimzuii mtunzi kuwatumia wahusika watu wazima au viumbe wengine. Watoto hupenda wahusika wanaofanana na wao na wenye hisia na uzoefu unaofanana na wao (Blaska, 2004). Aidha, watoto, hufurahia sana wanapowaona watoto wenzao wakiwa watendaji kutokana na huvutiwa sana na tabia za wahusika. Hupenda kujua nani mbaya na nani mzuri, kipi ni cha ukweli na kipi ni cha uongo, kipi kizuri na kipi kibaya.

2.3 Fasihi ya Watoto Huwa na Visa vichache

Tofauti na kazi za watu wazima kama vile tamthiliya ya *Kifo Kisimani* na riwaya ya *Vipuli vya Figo*, *Walenisi* na *Janga Sugu la Wazawa* kuwa ndefu kutokana na

kuwa na maonyesho au visa vingi ambavyo pia ni changamani vinavyoibuliwa na wingi wa migogoro, katika kazi za watoto zilizochunguzwa visa ni vichache kwa sababu pia migogoro ni michache. Aidha, visa hivi pia si changamani kwa maana kwamba mtoto anaweza kukifuatilia kisa kimoja kuanzia mwanzo hadi mwisho bila kuingiliwa na kisa kingine. *Tabu wa Taire* ni moja kati ya hadithi za watoto ambazo zina visa vichache, na ambavyo vimejengwa juu ya mhusika mkuu Tabu. Mhusika huyu, ni mtoto wa kikebaye alikuwa mtundu na alikatazwa mara nyingi na mama yake kwenda kucheza mbali na nyumbani. Tabu hakupenda kuzingatia maonyo ya mama yake. Badala yake anakwenda kucheza na huko anakamatwa na mpiga ngoma na kufungiwa ndani ya ngoma na kutumiwa kama kivutio cha mpiga ngoma kujipatia fedha. Baada ya siku nyingi kupita hatimaye Tabu anakuja kuokolewa na dada zake na mwisho Tabu anaazimia kutocheza tena mbali na nyumbani. Msuko wa aina hii wa visa unatokana na ukweli kwamba, watoto tofauti na watu wazima hawana uwezo wa kuelewa wala kukumbuka mambo mengi (Lan, 2013). Visa vikiwa vingi mtoto hushindwa kufuatilia ujumbe uliokusudiwa kutolewa na mwandishi, na hata kuacha kukisoma kitabu husika. Uchache wa visa hutegemea pia ngazi ya mtoto. Visa vinapokuwa vingi, wahusika au watendaji pia huwa wengi, na pia kunakuwapo na uchangamano mkubwa zaidi. Mara nyingi visa hivi hujengwa juu ya mhusika mkuu.

2.4 Kazi za Fasihi ya Watoto Hutumia Lugha rahisi/nyepesi

Tofauti na kazi za fasihi ya watu wazima ambazo huwa na lugha ngumu isiyofungwa na kanuni ya matumizi ya tamathali zozote zile za semi, lugha katika fasihi ya watoto huwa ni rahisi ila yenye mvuto kulingana na ngazi ya mtoto¹. Katika vitabu vilivyochunguzwa, ambavyo vinatofautiana ngazi, imeonekana kuwa kitabu cha ngazi ya kwanza kina lugha rahisi zaidi kuliko kitabu cha ngazi ya pili na tatu. Suala hili linamfanya mtoto aweze kufuatilia kisa bila kukwamishwa na kipengele hiki (Kahigi, 1995). Kitabu cha ngazi ya kwanza kina sentensi chache na rahisi ikilinganishwa na vya ngazi nyingine.

Umuhimu wa lugha katika vitabu vya watoto pamoja na mitindo inayotumika katika fasihi ya watoto kuwa rahisi na ya kuvutia ili iendane na kundi hili, pia ili kufanikisha kusudio la mwandishi (Kahigi 1995; Nodelman, 2008). Mtunzi wa kazi ya fasihi ya watoto lazima abuni na atumie mbinu rahisi za uwasilishaji ambazo hazitamchosha mtoto (Kahigi, 1995) kama vile uteuzi wa maneno ambayo yako wazi na rahisi (Nodelman, 2008). Lugha rahisi huchangia katika kumfanya mtoto aweze kufuatilia na hatimaye kuelewa kile kilichokusudiwa na mtunzi wa kazi husika bila kuchoka haraka. Mwandishi anatakiwa aepuke lugha ya mafumbo na yenye tamathali za semi hasa kwa

¹ Kwa mujibu wa Mradi wa Vitabu vya Watoto, vitabu vinaweza kugawanywa katika ngazi tatu. Ngazi ya kwanza hujumuisha darasa la kwanza na la pili. Ngazi ya pili darasa la tatu na la nne. Ngazi ya tatu darasa la tano hadi la saba.

watoto wa ngazi ya kwanza. Pia, sentensi ya kwanza idokeze kitu kinachofuata (Nodelman, 2008) ili kila wakati wanapoanza kusoma waweze kupata shauku ya kufuatilia kile kinachofuata. Lugha yenye mvuto na taharuki ni muhimu sana katika fasihi ya watoto. Lugha ya kwenye vitabu vya watoto lazima iwe rahisi na iendane na lugha anayozungumza mtoto na anayoisikia kwa watu wanaomzunguka. Hata hivyo, urahisi wa lugha pamoja na vipengele vya kumvuta mtoto, humjengea msisimko na udadisi hutegemea ngazi ya mtoto.

2.5 Hujengwa katika Msuko sahili wa Matukio

Msuko ni mtiririko wa matukio na mfuatano wake jinsi yanavyosimuliwa kuanzia tukio la kwanza hadi la mwisho ambao hujikita katika usababishi (Cuddon, 1992). Msuko wa matukio au ploti, katika fasihi ya watoto huwa sahili. Kwa mfano, katika hadithi ya *Bahati na Mumewe* tunaoneshwa maisha ya Bahati nyumbani kwa wazazi wake, jinsi anavyokataa wachumba wa mwanzo wa kijijini kwao na mwisho anapoolewa na mume kutoka nchi ya mbali na hali hatarishi anayokutana nayo hadi kutoroka kurudi nyumbani kwao. Watunzi hutofautiana katika kazi zao kutegemeana na hadhira inayoandikiwa, mada, itikadi, mtindo na kadhalika. Tofauti na watu wazima, watoto hupenda kuona visa vikitokea kimfuatano na kiwakati ili kuweza kufuatilia kile kinachoelezwa (Lyimo, 2014). Kutokana na hulka hii, watunzi wa kazi za watoto hujikita nao wakisana kazi zao kwa kuzingatia msuko wa matukio ambao ni sahili. Wahusika hawaelezwi kwa kina, wala kwa mapana, na badala yake, vitendo halisi vya wahusika, yakiwepo maneno wanayoyasema wao ndiyo yanayojenga kisa chenyewe.

2.6 Hutumia sana Fantasia

Fasihi ya watoto hutumia sana fantasia kama mbinu ya uwasilishaji. Fantasia kama anavyofafanua Lyimo (2014) ni mbinu ya kutumia njozi, nguvu za ajabu, na vipengele vingine vinavyoeleza mambo nje ya uhalisia. Aidha, ni sanaa ambayo mjengo wake umesheheni mambo ya kiajabuajabu, kinjozi, majitu ya kutisha, nguvu za ajabu. Matukio hutokea nje ya kanuni na sheria zilizopo ulimwenguni; uajabuajabu ndio hutawala na mara nyingi huhusisha safari na jasura (msako, utafutaji).

Tofauti na watu wazima, watoto hupenda vitu vihuishwe. Vitu kuongea au kutenda ni kawaida sana katika kazi za watoto. Aidha, huvutiwa sana na mambo ya ajabuajabu ambayo hayawezekani kutokea katika ulimwengu halisi. Mathalani, katika vipindi vingi vya watoto vinavyorushwa kupitia televisheni, watoto hupenda sana kuangalia michezo kama ya kina Superman, BEN 10 na kadhalika, ambayo ni fantasia tupu. Michezo hii huteka sana usikivu wa watoto. Katika utafiti huu, kuna kazi nyingi ambazo zimesheheni fantasia. Hadithi za *Kalikalange Mtoto wa Ajabu*, *Safari ya Mzimuni*, *Kirisongo*, *Mji wa Mawe*, *Chifu*

Mahawanga, Mganga Pazi, na Bahati na Mumewe ni mifano ya hadithi ambazo zimesheheni fantasia. Kwa mfano, katika hadithi ya *Kalikalange Mtoto wa Ajabu* kuna fantasia mbalimbali. Mtoto wa ajabu ambaye kabla ya kuzaliwa anazungumza na kusema kuwa anataka kutoka. Aidha, anatoa maelekezo ya nini wanajamii wafanye ili aweze kuzaliwa. Wanajamii pamoja na kuwa wao wana uelewa zaidi ya mtoto, wanakubaliana na maagizo anayoyatoa mtoto Kalikalange. Fantasia kuhusu mtoto *Kalikalange* bado inaendelea hadi kuoneshwa akikaangwa kwenye chungu, na jinsi alivyopambana na majitu ya ajabu na kuyashinda akiwa bado mtoto mdogo. Katika hali ya kawaida au ulimwengu halisi, haya ni mambo ambayo hayawezezekani kutokea.

Pamoja na kuwa fantasia huchukuliwa kama mbinu ya uwasilishaji wa mambo yasiyowezezekana, ni mtindo ambao una dhima anuwai (Cooper 1984, Yanarella na wenzie 1988, Williams 1975). Kwa mujibu wa Leeson (1984), fantasia ni mtindo wa kiuandishi ambao ni wa kifilosofia zaidi, kiitikadi zaidi na kisiasa zaidi na ni kutokana na fantasia mtoto anapata mawazo kuhusu jinsi dunia inavyopasa kuwa. Aidha, baadhi ya kazi za kifantasia kwa mujibu wa Cooper (1984), husaidia katika kuimarisha tamaduni za wanajamii kwa hujenga taswira kupitia visasili na visakale na kadhalika na hivyo kusaidia katika kujenga utambulisho wa wanajamii kama jumuiya au taifa moja. Watoto, tofauti na watu wazima, kutokana na ufahamu wao mdogo wa kiulimwengu, huamini kuwa, mambo hayo ya ajabu ni ya kweli na hivyo huyafurahia sana. Kutokana na kusoma kazi kama za *Kalikalange Mtoto wa Ajabu*, mtoto mbali na kufurahia hadithi, hujifunza mambo mbalimbali kama vile ya kujiamini, ushujaa, upelelezi na udadisi.

2.7 Huhusisha Milango mbalimbali ya Fahamu

Mtunzi wa kazi ya fasihi ya watoto tofauti na wa fasihi ya watu wazima, hutumia sambamba na lugha vitu vinavyohusisha milango ya fahamu. Mathalani, matumizi ya picha, rangi, milio, namna ya kufanya kitu, uhuishaji na kadhalika humjengea mtoto ambaye ndiye mlengwa mkuu picha halisi akilini (Nodelman, 2008) kumsaidia katika kuhifadhi kumbukumbu pamoja na kumvutia mtoto. Ni kawaida kwa fasihi ya watoto (hasa wa umri wa miaka 0-5) kutawaliwa zaidi na picha zenye rangi mbalimbali (hasa zinazong'aa) au michoro pamoja na milio, tofauti na ilivyo kwa fasihi ya watu wazima. Vitu hivi haviwekwi kwa bahati mbaya bali hutokana na dhima yake kuu kwamba, watoto huuelewa ulimwengu kwa njia hii (Narahara, 1998). Kwa ujumla, watoto hupenda kusikia milio, kuona vitu, kunusa harufu, kugusa na si kwa maneno matupu tu. Mtunzi wa kazi za watoto huhakikisha kuwa picha, vielelezo na lugha inayotumika vinahusisha milango yao ya fahamu, hata kama si milango yote. Kwa mfano katika hadithi ya *Tamaa ya Chura* tunasikia sauti mbalimbali za vyura wakikoroma. Sauti hizo ni tofauti. Mwandishi anaweka sauti tofauti za vyura; wakati wakikoroma na wakati walipokuwa wakiyafurahia maji. Hapa mtoto anawezeshwa kusikia sauti za

vyura, tena sauti tofauti. Katika fasihi ya watu wazima ingetoshwa tu kuonesha kuwa vyura walikoroma na kuimba kwa furaha walipokuwa wakiyafurahia maji. Kuweka sauti kama hizi kwenye fasihi ya watoto ni kumfanya mtoto aamini kuwa yale yanayoelezwa na kutendeka ni mambo ya kweli.

2.8 Maisha ya Wahusika Huanzia na Kuishia Nyumbani

Watafiti wa fasihi ya watoto wanaeleza kuwa, wahusika wa kazi za watoto hususan wahusika wakuu, huanzia maisha yao nyumbani na huishia nyumbani (Nodelman, 2008). Hii inatokana na ukweli kuwa, watoto huwa ni watu ambao wako chini ya himaya na maelekezo ya wazazi au walezi kutokana na kuwa wategemezi au watu wasioweza kujimudu kimaisha. Iwapo mtoto ataondoka nyumbani bila kurudi huwa na tafsiri nyingine kama vile kukua; kwa maana ya kuanza kujitegemea, au kupotea na lazima jitihada za kumrudisha nyumbani zifanywe (mfano Tabu katika *Tabu wa Taire* na Bahati katika *Bahati na Mumewe*). Mathalani, Tabu ambaye ni mtoto alikuwa akionywa kila mara asicheze mbali na nyumbani. Tabu hakuzingatia maonyo haya. Kutokana na kukosa usikivu, mwisho anatekwa na mpiga ngoma na anaondoka naye huku akiwa amewekwa ndani ya ngoma. Pamoja na kukosa usikivu, wazazi na wanajamii wanashirikiana kumtafuta Tabu na hatimaye anapatikana na kurudishwa nyumbani huku mpiga ngoma akiadhibiwa. Katika hadithi ya *Bahati na Mumewe* tunamwona Bahati akishauriwa aolewe na watu ambao wanafahamika. Bahati anawakataa wachumba wote wa eneo analoishi na kuamua kuolewa na mtu wa mbali. Matokeo yake baada ya kufika katika nchi ya mbali, anagundua kuwa mume wake hakuwa binadamu na kwamba alikuwa anasubiri siku ya kumua Bahati. Kabla ya kufikia azma hiyo, Bahati anafanikiwa kuelezwa siri hii na anatoroka na kurudi tena nyumbani kwa wazazi wake na hivyo kuepuka kifo. Hadithi za aina hii zipo kwa ajili ya kuonesha kuwa mtoto anapaswa kuwa katika uangalizi kwa ajili ya usalama hadi atakapoweza kufanya maamuzi sahihi au kujitegemea kimaisha. Katika vitabu vingi vya watoto hata kama mtoto ataondoka nyumbani, mwisho anaonekana kurudi nyumbani.

2.9 Mambo mema ndiyo Yatarajiwayo

Fasihi ya watoto hulenga kuwapatia watoto mambo mema (Nodelman, 2008), hivyo mtunzi wa kazi za watoto husana kazi yake ambayo itaelekeza katika matarajio au matazamio mema. Ijapokuwa kazi nyingi za watoto huwa zimejengwa katika kuonesha uzuri na ubaya, mara nyingi kazi hizi huonesha kuwa wema ndio unaoshinda na ndio unaotakiwa. Hivyo, pamoja na kuwapo kwa mchanganyiko wa mambo mema na mabaya, mema ndiyo hasa mtunzi huyakusudia ili yawafikie walengwa. Kwa mfano, katika hadithi ya *Chifu Mahawanga*, binti Namikoha ambaye ni binti mdogo wa Mzee Ngayombotele na

mkewe Mholeli alifanikiwa kuwa mke wa chifu kutokana na kuwa mtiifu, msikivu na mnyenyekevu. Tabia hizi zilimsaidia na akaweza kufuata taratibu zilizokuwa zinapaswa kufuatwa na binti yeyote ambaye angetaka kuolewa na chifu. Binti mkubwa, Nanjengi, alishindwa kuwa mke wa chifu kutokana na tabia yake ya kiburi na kutokuwasikiliza wakubwa wake. Aidha, aliuawa na joka na ukawa mwisho wa maisha yake na kiburi chake. Kutokana na hadithi hii, watoto hujifunza kuwa watiifu wakiadini kufanikiwa katika mambo mengi, na huogopa kuwa wakaidi ili kuepuka yaliyompata Nanjengi.

2.10 Hukusudiwa Kutoa Mafundisho au Maadili kwa Mifano

Lengo la fasihi ya watoto mbali na kuburudisha ni kuwafundisha watoto (Nodelman, 2008). Fasihi ya watoto hukusudiwa katika kutoa fundisho au adili fulani. Fundisho hili huwa limejengwa au kushehenezwa mafundisho mbalimbali kwa watoto kuhusu masuala anuwai yanayowahusu wao, tabia zinazokubalika katika jamii kwamba wazifuate na kuacha tabia ambazo hazikubaliki katika jamii kama vile uchoyo, ulafi, ukaidi, uvivu, wizi na kadhalika. Mafunzo hutofautiana kulingana na ngazi au umri wa mtoto. Mara nyingi baada ya hadithi fulani, watoto huulizwa kuhusu funzo linalotokana na hadithi waliyoisoma au waliyosimuliwa. Katika hadithi ya *Wawindaji Watatu*, mwandishi anaanza kumwonesha mtoto Ali kuwa alikuwa mchoyo, tabia ambayo ilimkera sana mama yake. Ili kumfanya Ali aondokane na tabia hiyo, anaingiza hadithi ya wawindaji. Hadithi hii ina mambo mengine mabaya yakiwamo ya kuwekeana sumu na kuuana kwa sababu ya kila mmoja kutaka pesa walizopewa ziwe zake. Hatimaye wanakufa wote na wanazikosa zile fedha. Hadithi hii inamfunza mtoto kwa mifano dhahiri au ya kuaminika.

2.11 Hutumia Mbinu ya Kurudiarudia

Fasihi ya watoto huwa ina mtindo wa kurudia maneno, tungo, hali, mazingira hata ruwaza za usimulizi (Nodelman, 2008) kujitokeza kwa aina ya wahusika, lugha, muundo na kadhalika. Kwa mujibu wa wataalamu wa fasihi, marudio ni sifa mojawapo kuu ya fasihi simulizi (Nodelman, keshatajwa) hivyo fasihi simulizi ni malighafi ya fasihi andishi ya watoto hasa kwa upande wa hadithi fupi na riwaya kutokana na fasihi andishi ya watoto kuchota mambo mengi kutoka fasihi simulizi. Kwa kutumia hadithi ya *Bahati na Mumewe* (1995: 1) tunaweza kuona mfano wa marudio haya:

Japokuwa Bwana Jojo na mkewe walichelewa kupata mtoto, hatimaye Mungu aliwajalia mtoto wa kike. Walimpa jina Bahati. Mtoto huyo alikuwa mzuri. Marafiki, majirani na ndugu za Bwana na Bibi Jojo walifika kumwona mtoto Bahati... Naam, nyumbani kwa Bwana Jojo na mkewe, sasa Baba na Mama Bahati, kulikuwa na furaha.

Lengo la kutumia mtindo kama huu ni kuwafanya wasomaji wazame na kufuatilia kile kinachowasilishwa. Kwa vile watoto huwa wanaweza kufanya mambo mengi kwa wakati mmoja, marudiorudio ya jina 'Bahati' na 'mtoto Bahati' yanamsaidia mtoto aweze kufuatilia kile kinachoelezwa vizuri na kama njia ya kumkumbusha kile kinachoelezwa.

2.12 Kazi za Fasihi ya Watoto Hutumia sana picha na Michoro

Katika kazi za watoto zilizochambuliwa kulikuwa na matumizi makubwa ya picha kwenye jalada la kila kitabu na ndani ya kitabu. Kwa upande wa vitabu vya watu wazima vilivyochambuliwa, vitabu vyote vitano vina picha kwenye jalada. Kati ya vitabu hivi, vitabu vinne havina picha nyingine yoyote ndani ya kitabu. Kitabu kimoja tu (Mzimu wa Watu wa Kale) ndicho chenye picha ndani ya kitabu. Kwa hali hii ni wazi kuwa matumizi ya picha ni nduni bainifu katika vitabu vya fasihi ya watoto.

3.0 Hitimisho

Makala haya yamejaribu kubainisha nduni za fasihi andishi ya watoto. Kwa kiasi kikubwa imejikita katika kuchunguza zaidi fani katika kazi za fasihi ya watoto zilizochambuliwa. Kwa kuwa fasihi ya watoto nchini Tanzania bado ni changa kutokana na kukosekana kwa tafiti nyingi, tafiti zaidi zinahitajika kuhusiana na fasihi hii, ikiwa ni pamoja na kupata marejeleo yanayohusu fasihi ya watoto. Lengo la kuhitajika huku kwa tafiti kama hizi ni kutokana na ukweli kwamba, watoto hutofautiana na watu wazima hasa katika vionjo vya furaha na huzuni, ustahimilivu, kufikiri, kuguswa na kadhalika na kwa njia hii, fasihi ya watoto inao upekee ambao hauna budi kubainishwa.

Marejeo

- Abdulla, M. S. (1974). *Mzimu wa Watu wa Kale*: Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Blaska, J. K. (2004). "Children's Literature that Includes Characters with Disabilities or Illnesses". *Disability Studies Quarterly Winter 2004*, Juzuu 24, Na. 1 iliyosomwa toka <http://dsq-sds.org/article/view/854/1029> tarehe 8 Februari 2013.
- Abeid, M. (1996). *Mji wa Mawe II*, Dar es Salaam: M & K Publishers and Agencies Limited.
- Bwana, J. H. (2003). *Mganga Pazi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.

- Cooper, S. (1984). "Escaping into Ourselves". Katika Robert, H. Boyer and Kenneth J. Zahorski (wah.). *Fantasists on Fantasy*. New York: Avon. 282-292.
- Cuddon, J.A., (Mh.). (1992). *The Penguin Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*. Harmondsworth: Penguin
- Dumea, P.H. (2006). *Chifu Mahawanga*. Dar es Salaam: Readit Books Ltd.
- Ebraju, P.B. (1999). *Sababu Mimi ni Mwanamke!* Dar es Salaam: Educational Books Publishers Ltd.
- Kahigi, K.K. (1995). "Lugha katika Vitabu vya Watoto" *Kioo cha Lugha*, Juzuu 1/1. Dar es Salaam: Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. 21-35.
- Kayoka, C. (1998). *Kalikalange Mtoto wa Ajabu*. Dar es Salaam: HEKO Publishers Ltd.
- Kwalazi, E.T. (2006). *Tabu wa Taire*. Dar es Salaam: Readit Books Ltd.
- Lan, L. (2013). *Nyimbo za Kiswahili za Watoto*. Kazi Maalum, SW 399, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Lingindo, R.M.K. (2000). *Wawindaji Watatu*. Dar es Salaam Oxford University Press (T) Ltd.
- Lyimo, E.B. (2014). *Usaguzi wa Kijinsia katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto na Mtazamo wa Wadau Nchini Tanzania*. Tasinifu ya PhD. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Lotto, M.M. (1999). *Laba Msichana Shujaa*. Dar es Salaam: HEKO Publishers Ltd.
- Mateso, C. (1998) *Safari ya Mzimuni*. Dar es Salaam: Readit Books Ltd.
- Mberia, K. (2001) *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.
- Mbogo, E. (1996) *Vipuli vya Figo*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Mghanga, M. (2002). *Kirisongo*. Dar es Salaam: Centre for Democratic and Strategic Management.
- Mkangi, K. (1995) *Walenisi*. Dar es Salaam: Ujuzi Educational Publishers Ltd.
- Mkufya, W.E. (2006). *Tamaa ya Chura*: Dar es Salaam: Mangrove Publishers.
- Msuazi, J. (2009). *Sara na Kaka Zake*. Dar es Salaam: Stadium Educational Investments Limited.
- Mtobwa, B.R. (1998). *Kipofu Mwenye Miwani Myeusi*. Dar es Salaam: HEKO Publishers Ltd.
- Mulokozi, M.M. (1989). "Uchambuzi wa Mashairi", *Mulika* 21: 48-59
 _____ (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mwenda, D. (1995). *Bahati na Mumewe*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.
- Narahara, M.N. (1998). "Gender Stereotypes in Children's Picture Books". *Exit Project EDEL 570*, University of California, Long Beach.

- Nodelman, P. (2008). *The Hidden Adult: Defining Children's Literature*
Baltimore, Md.: Johns Hopkins University Press.
- Ruhumbika, G. (2001). *Janga Sugu la Wazawa*. Dar es Salaam: E&D Limited
- Ruterana, P.C. (2012). Children's Reflection on Gender Equality in Fairy Tales:
A Rwanda Case Study, *The Journal of Pan African Studies*, vo. 4 no.9,
January, pp85-101.
- Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus
Books.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Kiswahili*.
Nairobi: Vide – Muwa Publishers Ltd.